**(IJA)**
**CHUO CHA UONGOZI WA MAHAKAMA**
**LUSHOTO**

# HOTUBA YA MWENYEKITI WA BARAZA LA UONGOZI WA CHUO MHE. JAJI DKT. GERALD A.M. NDIKA KWENYE SHEREHE YA MAHAFALI YA 19 YA CHUO CHA UONGOZI WA MAHAKAMA LUSHOTO TAREHE 29 NOVEMBA, 2019 YALIYOFANYIKA KWENYE UKUMBI WA NYALALI, IJA - LUSHOTO

Jaji Mkuu wa Tanzania, Mheshimiwa Profesa Ibrahim Juma;

Waheshimiwa Majaji Wafawidhi Mahakama Kuu Kanda ya Tanga na Moshi;

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo;

Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya,

Wajumbe wa Baraza la Uongozi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto mliomaliza muda wenu;

Viongozi Waandamizi wa Chuo,

Viongozi mbalimbali wa Serikali;

Wahadhiri na Watumishi wote wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto;

Wazazi, Walezi, Ndugu na Marafiki wa Wahitimu wetu;

Wageni Waalikwa;

Wahitimu wote waliosoma IJA ambao wamehudhuria Mahafali ya leo;

Wapendwa Wahitimu wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto,

Mabibi na Mabwana,

Habari za Asubuhi.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** sina budi nami kuchukua fursa huu kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametupa tunu ya uhai na afya njema ambayo imetuwezesha kuja katika hadhara hii mahsusi ya shamrashamra za Mahafali ya Kumi na Tisa ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto. Kwa niaba ya Baraza la Uongozi wa Chuo na Wanajumuiya wote wa Chuo, naungana pia

na Mkuu wa Chuo kukukaribisha wewe pamoja na kukushukuru kwa namna ya pekee kwa kukubali mwaliko wetu wa kuwa Mgeni Rasmi katika Mahafali haya ya Kumi na Tisa (19). Hii ni uthibitisho tosha unaonyesha kwamba Chuo hiki si tu ni sehemu ya Mahakama ya Tanzania bali pia ni muhimu katika kusaidia Mahakama kutimiza wajibu wake wa kutoa haki sawa na kwa wakati kwa wote.

Uwepo wako kwenye Sherehe hizi adhimu ambazo huadhimishwa kila mwaka ni faraja tosha kwa wahitimu wetu ambao leo hii utawatunuku vyeti vyao.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** nami pia natambua wingi na uzito wa majukumu yako kitaifa ukiwa ni Jaji Mkuu wa Mahakam ya Tanzania, hivyo ujio wako umeonesha ni jinsi gani unazithamini Taasisi zilizo chini ya Mahakama ya Tanzania kikiwemo Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto. Nachukuwa fursa hii kukushukuru na kukukaribisha. **Karibu sana.**

Aidha, naomba pia niungane na Mkuu wa Chuo kuwakaribisha viongozi mbalimbali, wageni waalikwa, wazazi, ndugu na marafiki wote ambao mmetuthamini na kuacha kazi zenu ili kujumuika nasi katika mahafali haya.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** kama alivyoeleza Mkuu wa Chuo hivi punde, tunaposherehekea Mahafali haya ya Kumi na Tisa, jumla ya wahitimu **6037** wamehitimu katika ngazi ya Stashahada na Astashada ya Sheria tangu kilipoanzisshwa na kuanza kutoa mafunzo hayo mwaka 2001. Idadi hiyo ya wahitimu miongoni mwao wameajiriwa kama maafisa kumbukumbu wasaidizi katika Mahakama ya Tanzania na

ambao baadhi yao wamejiendeleza na wamepanda hadi kufikia ngazi ya naibu wasajili. Wapo pia miongoni mwao ambao huajiriwa katika serikali kuu kama watendaji wa Vijiji (VEO) na watendaji wa Kata (WEO). Pamoja na hilo, wahitimu wetu wengi wa Stashahada ya Sheria wamekuwa wakipata nafasi ya kujiunga katika vyuo vikuu mbalimbali vya serikali na binafsi kuendelea na masomo yao ya Shahada ya Sheria na wale wa Astashahada ya Sheria wengi wao wanaendelea na masomo ya Stasahahada ya Sheria.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** Aidha katika utoaji wa elimu bora, Chuo kwa sasa kina jumla ya wanataaluma ishirini na moja (21) ambao wameendelezwa na kuwezesha Chuo kupata mafanikio ya kitaaluma yaliyotajwa.

Miongoni mwa wanataaluma hao ishirini na moja (21), wanne (4) wana Shahada ya Uzamivu na kumi na saba (17) wana shahada ya Uzamili. Kwasasa kati ya hao 17, watatu (3) wanaendelea na mafunzo ya Shahada ya Uzamivu. Katika kuendeleza wanataaluma, katika Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (2018/19-2022/23) Chuo kina mpango wa kupeleka wanataaluma wengine wane kwa ajili ya mafunzo ya Shahada ya Uzamivu.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** kama alivyotangulia kusema Mkuu wa Chuo, tukiwa ni taasisi ya Mahakama inayoratibu, kusimamia na kuendesha mafunzo kwa watumishi wa kada mbalimbali za Mahakama, tumeendelea kuboresha utendaji wa **Kurugenzi ya Mafunzo Endelevu ya Kimahakama.** Kurugenzi hii imeendelea kufanya kazi kwa karibu na kitengo cha mafunzo cha Mahakama kuratibu na kuendesha mafunzo ya muda mfupi,

yaani semina, warsha, mafunzo ya wakufunzi na kozi nyinginezo fupi za kuwaongezea weledi watumishi wa ngazi zote wa Mahakama ya Tanzania. Hii ikiwa ni pamoja na mafunzo ya wadau wa Mahakama ambao ni Madalali na Wasambaza nyaraka wa Mahakama.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** nichukue fursa hii tena kwa niaba ya Baraza la Uongozi wa chuo kutoa shukrani za pekee kwako Mhe. Jaji Mkuu, Mhe. Jaji Kiongozi, Mtendaji Mkuu wa Mahakama pamoja na Msajili Mkuu kwa kuendelea kutoa ushirikiano wenu kwa Uongozi wa Chuo, kwa kutoa kipaumbele kwa shughuli za Chuo hususan kutenga fedha za mafunzo kwa maafisa wa mahakama na wasaidizi wao nchini na kuendelea kukiamini Chuo kuratibu mafunzo hayo ambayo yanaendelea kutolewa hapa chuoni.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** yatosha tu kusema kwamba, mafanikio ambayo Mkuu wa Chuo ameyaeleza kwenye nyanja ya utafiti na mafunzo kwa watumishi wa mahakama na wadau wake kwa kiasi kikubwa tumeyafikia kutokana na ushirikiano wenu wa dhati ambao tumeupata si tu kwenu ninyi bali pia kwa Majaji Wafawidhi wa kanda zote za Mahakama Kuu nchini ambao wamekuwa ni sehemu ya mafanikio tuliyoyapata katika kufikia malengo yetu. Tunaushukuru sana uongozi wa Mahakama ya Tanzania kwa kukiamini chuo chetu kuwa kinaweza kutekeleza majukumu haya makubwa.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** kama alivyobainisha Mkuu wa Chuo kwenye maelezo yake, tunajitahidi kutekeleza Mpango Mkakati kila uchao kwa kadri ya uwezo wetu. Katika kutekeleza lengo mahsusi la kutoa ushauri wa kitaalamu *(consultancy),* Chuo

kiliweza kushinda zabuni iliyotangazwa na Shirika la umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO) la kuandaa muongozo wa kufundishia na kuendesha mafunzo kwa mkoa wa Morogoro na hususan kwenye wilaya za Mvomero na Kilosa.

Aidha, tunapenda kukufahamisha kuwa, utekelezaji wa mikakati iliyoainishwa katika Mpango Mkakati wa Chuo wa Miaka Mitano itategemea kwa kiasi kikubwa pamoja na mambo mengine upatikanaji wa mapato ya ndani na fedha za maendeleo na ruzuku kutoka Serikalini. Hivyo basi, kwa heshima kubwa tunaendelea kuomba Mahakama ya Tanzania, Taasisi unayoiongoza kuangalia uwezekano wa kutupatia fedha ya maendeleo ili tuweze kumaliza ujenzi wa jengo la hosteli ya wanafunzi wa kiume fedha ambayo haijawahi kuletwa kwa miaka zaidi ya mitano sasa.

Ninaomba kutumia nafasi hii kukuhakikishia kuwa Baraza la Uongozi wa Chuo lina mkakati mahsusi wa kuinua hadhi ya Chuo kwa kushirikiana na Menejimenti ili kukifanya Chuo kuwa na heshima na hadhi ya kitaifa na kimataifa kwa kutoa mafunzo mbalimbali katika nyanja ya utoaji haki na utawala wa sheria.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**, kwa niaba ya Baraza la Uongozi wa Chuo tunaendelea kuiomba serikali ili iendelea kuajiri wahitimu wetu ambao ni mahiri waweze kuajiriwa katika Mahakama zetu kwa ngazi mbalimbali, kwenye serikali kuu kama Watendaji wa kijiji na Watendaji wa Kata pamoja na nafasi nyinginezo katika Wizara, Taasisi na Mashirika ya Umma. Mbali na tasnia hii ya sheria, wahitimu wetu huwa wanafundishwa maadili ya Utumishi wa Umma na maadili ya kitaaluma katika fani ya

sheria na hivyo wameandaliwa vyema kwa ajili ya ajira katika Utumishi wa Umma.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** baada ya maelezo hayo nami nichukue nafasi hii kwa niaba ya Baraza la Uongozi wa Chuo kuungana na Mkuu wa Chuo kuwapongeza wahitimu wetu ambao leo hii wanatunukiwa Stashahada na Astashahada ya Sheria hapa chuoni. **Hongereni sana.**

Ndugu Wahitimu, naomba ninukuu moja ya misemo ya hekima ya Rais wa Kwanza wa Afrika Kusini, Hayati Nelson R. Mandela kwamba: '**Education is the most powerful weapon which you can use to change the world'** akiwa na maana **'Elimu ni silaha yenye nguvu kuliko zote unayoweza kuitumia kubadilisha dunia.'** Mimi kama mzazi, ninawasihi wahitimu wetu wauenzi na kuuishi kwa vitendo usemi huu kwa kuitumia elimu waliyoipata hapa kuwa ni chachu ya kuibadilisha dunia kwenye mwelekeo chanya katika nyanja zote za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Naamini kabisa elimu waliyoipata hapa Chuo wataitumia kwa kuleta mabadiliko makubwa katika taifa letu na dunia kwa ujumla.

Pia, niendelee kuwaasa wahitimu wetu kuwa sio rahisi kwamba wataweza kulipa fadhila za wazazi au walezi wao ambao wametoa mchango uliowawezesha kuhitimu mafunzo yao leo hii. Hivyo basi, hawana budi kuendelea kuwashukuru wazazi, walezi na watanzania kwa ujumla kwa kutumia utaalamu na ujuzi walioupata hapa Chuoni kama nyenzo muhimu ya kufanikisha maisha yao binafsi, ya familia, jamii na Taifa kwa ujumla. Lakini pia, Kama ilivyo ada ya wahitimu waliotangulia, tunawaomba wawe mabalozi wetu wazuri wa kukitangaza chuo na

kushirikiana na chuo kupitia jumuiya ijulikanayo kama ***IJA Alumni Association*** ambayo mara tu baada ya kutunukiwa Stashahada na Astashahada ya Sheria watakuwa wanachama rasmi wa jumuiya hii muhimu.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** ninaomba sasa kuhitimisha hotuba yangu kwa kukushukuru tena kwa mara nyingine kwa kukubali kuja kushiriki nasi leo. Kwa niaba ya Baraza la Uongozi wa Chuo, tunakutakia heri na mafanikio makubwa katika majukumu yako makubwa ya kitaifa ya kuongoza Mahakama ya Tanzania.

Ni matumaini ya Baraza la Uongozi wa Chuo kwamba katika kipindi chako cha Uongozi utaendele kukilea na kukiwezesha Chuo hiki kutimiza malengo yake na kukiwezesha kuwa kituo muhimu na cha pekee cha Mafunzo Endelevu ya Kimahakama na hususani kuwa Chuo bora cha Mahakama Afrika Mashariki na Kimataifa kama dhima ya Chuo hiki ilivyo.

**Mwisho,** ninaomba niwashukuru tena wageni waalikwa waliohudhuria sherehe hii, wahitimu, wazazi, walezi wote mliopo hapa kwa kukubali kushirikiana nasi katika tukio hili. Nawatakieni heri katika kusherehekea tukio hili muhimu na hatimaye mrejee salama salimini kwenye makazi yenu.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**, ninaomba sasa kwa heshima na taadhima nikukaribishe ili uweze kuongea na hadhara hii ya Mahafali ya 19 ya Chuo chetu.

**Asanteni kwa kunisikiliza.**

**IJUMAA, 29 NOVEMBA 2019**